JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE

**Kumb. Na.HWK/S.1/24/Vol.III/174** **24/05/2021**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe anatangaza nafasi (4) za kazi. Tangazo hili limetokana na barua **Kumb. Na. FA.97/228/01/9 ya tarehe 13 Mei, 2022** kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ikihusu idhini ya kutekeleza ikama na bajeti kwa ajira mpya katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Maombi ya kujaza nafasi yoyote kati ya hizo yanakaribishwa kutoka kwa Mtanzania yoyote mwenye sifa zilizotajwa katika Tangazo hili:

1. **KATIBU MAHSUSI DARAJA LA III- NAFASI MBILI (2)**

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

i. Awe na elimu ya kitado cha IV
ii. Awe amehudhuria mafunzo ya Uhazili na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu
iii. Awe amefaulu somo la Hatimkato na Kingereza kwa maneno 80 dakika moja
iv. Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka Chuo chochote kinachotambulika na Serikali na kupata Cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, Email na Publisher

**MAJUKUMU YA KAZI.**

i. Kuchapa barua, taarifa na nyaraka za kawaida
ii. Kusaidia kupokea Wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
iii. Kusaidia kutunza kumbukumbu/ taarifa za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine.
iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake majalada, nyaraka au kitu chochote kinachohitajika katika shughuli za kazi hapo ofisini
v. Kusaidia kufikisha maelekezo ya Mkuu wake wa kazi kwa Wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu taarifa zozote atakazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
vi. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maafisa walio katika sehemu alipo na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika
vii. Kutekeleza kazi zote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi

***Ngazi ya Mshahara TGS B kwa mwezi***

2. **DEREVA DARAJA LA II - NAFASI MBILI (2)**

**SIFA ZA MWOMBAJI:**

i. Awe na elimu ya kitado cha IV.
ii. Awe na Leseni ya Daraja E au C1 ya uendeshaji magari .
iii. Awe amefanya kazi kwa muda wa Mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
iv. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
v. Mwombaji mwenye cheti cha Majaribio Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**MAJUKUMU YA KAZI.**

i. Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.
ii. Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.
iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
vi. Kufanya usafi wa ngari na
vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake.

***Ngazi ya Mshahara TGS B kwa mwezi***

**NB: MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE:**

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kati ya miaka 18 hadi 45.
2. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) watatu wa kuaminika.
3. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya taaluma, maelezo binafsi, vyeti vya Kidato cha nne au kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa husika na Picha moja "Passport Size" ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.**Viambatanisho hivyo vibanwe sawa sawa kuondoa uwezekano wa kudondoka au kupotea.**
4. Kwa waombaji waliosoma nje ya nchi elimu ya kidato cha nne na/au kidato cha sita wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA).
5. Kwa waliohitimu elimu ya chuo nje ya nchi, wawasilishe uthibitisho kutoka Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE).
6. **Testimonials "Provisional Results" Statement of results; hati ya matokeo ya kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) HAVITAKUBALIWA.**
7. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.
8. Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi; wahusika watachukuliwa hatua za Kisheria.
9. Waombaji wote watakaokidhi vigezo ndiyo watakaoitwa kwenye usaili (Interview)

10. Maombi yasiyozingatia vigezo vilivyoanishwa hayatashughulikiwa.

11. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe ***09 Juni, 2022 saa 9:30 Alasiri*.**

12. Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza na barua ya maombi isainiwe na kuambatishwa na vielelezo vinavyohitajika na yatumwe kupitia posta kwa anuani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Halmashauri ya Wilaya,**
**S.L.P. 584,**
**Korogwe.**

Au

**District Executive Director,**
**Korogwe District Council,**
**P.O. Box 584,**
**Korogwe.**

**NB: Tangazo hili pia linapatikana kwenye Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe www.korogwedc.go.tz**

DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR
P. O. BOX 584,
KOROGWE

Halfan H. Magani
**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**